



# THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA

**A. M. E. C. E. A**

**LANGATA CAMPUS**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA**

**AGOSTI - DISEMBA 2014**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII**

**IDARA YA KISWAHILI**

**ED 314: MBINU ZA KUFUNDISHIA KISWAHILI**

P.O. Box 62157  
00200 Nairobi - KENYA  
Telephone: 891601-6  
Fax: 254-20-891084  
E-mail: academics@cuea.edu

**Tarehe: Disemba 2014**

**Muda: Saa Tatu**

**Maagizo: Jibu swali la kwanza na mengine Matatu**

- S1. a) Fafanua yafuatayo:
- i) Nadharia ya utabia **(Alama 2)**
  - ii) Silabasi **(Alama 1)**
  - iii) Mada ya Somo **(Alama 1)**
- b) Taja faida MBILI za maazimio ya kazi. **(Alama 2)**
- c) Eleza sababu NNE za kutayarisha mpangilio wa somo kabla ya kufundisha. **(Alama 4)**
- d) Eleza mbinu zozote TATU ambazo ungetumia kufundisha somo la mazungumzo. **(Alama 3)**
- e) Taja sifa NNE ambazo mwalimu anaweza kuzingatia katika uteuzi wa vitabu vya fasihi. **(Alama 4)**
- f) Bainisha sifa NNE za mwalimu bora wa Kiswahili. **(Alama 4)**
- g) Thibitisha maoni ya mwana isimu jamii Dell Hymes kwamba kujua sarufi ya lugha pekee sio kujua lugha. **(Alama 4)**
- S2. Jadili umuhimu wa matumizi ya vifaa katika kufundisha Kiswahili. **(Alama 15)**

- S3. Jadili njia mbalimbali za kutahini wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.  
**(Alama 15)**
- S4. Andaa somo la dakika 40 huku ukionyesha jinsi utakavyofundisha somo la matamshi.  
**(Alama 15)**
- S5. Umepelikwa kufundisha Kiswahili katika shule ya upili ya Mavueni, kidato cha pili. Fafanua maandalizi utakayofanya kabla ya kuanza kufundisha.  
**(Alama 15)**
- S6. “Mwalimu wa Kiswahili hukumbana na pingamizi nyingi katika kutekeleza ufundishaji wake.” Jadili kauli hii huku ukizingatia hali halisi zilizoko nchini Kenya.  
**(Alama 15)**

**\*MWISHO\***